# KLINIKI ZA SHERIA NJIA MPYA YA KUPUNGUZA KESI NA KUSOGEZA HAKI KWA WANANCHI

**Na Mwandishi wetu**

Katika jitihada za kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi wote, hususan wale wa kipato cha chini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzisha utaratibu wa kufanya Kliniki za Sheria katika Mikoa mbalimbali ili kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi. Utaratibu kwa kufanya Kliniki hizi umelenga kupunguza changamoto zinazowakabili wananchi pindi wanapohitaji msaada wa kisheria.

Akizungumza kuhusu mpango huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Uratibu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Ipyana A. Mlilo, anasema Kliniki hizo zimeanzishwa kwa kuzingatia kifungu cha 31 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 marejeo ya Mwaka 2023. Kupitia kifungu hicho, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametengeneza mwongozo unaowezesha kuundwa kwa Kamati za Ushauri wa Kisheria katika ngazi za Mikoa na Wilaya, zikiwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Kliniki hizo.

### Kusogeza Huduma kwa Wananchi

Kliniki za Sheria zimekuja kama suluhisho la changamoto ya muda mrefu ambapo wananchi wengi walikosa huduma za kisheria kutokana na gharama, umbali, na hofu ya urasimu. Kupitia mpango huu, wananchi wanapata fursa ya kusikilizwa bure, kupatiwa ushauri wa kisheria, na hata kusaidiwa kutatua migogoro yao bila kulazimika kufika mahakamani.

Kwa mujibu wa Bw. Mlilo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iligundua kuwa inakabiliwa na wimbi kubwa la kesi zinazofunguliwa dhidi yake, kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Kitaifa. Aidha Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekuwa akishtakiwa mara kwa mara kutokana na nafasi yake kama Mshauri wa Serikali katika masuala yote ya Kisheria.

Alisema kutokana na Serikali kushtakiwa Mahakamani mara kwa mara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitafuta mbinu mbadala ya kupunguza migogoro hiyo kabla haijafika mahakamani.

"Hatukuona busara kuendelea kusubiri hadi kesi zifike Mahakamani ambako baadhi yake Serikali inapoteza na kulazimika kulipa fidia. Ndipo tukaanzisha utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi mapema kupitia Kliniki za Sheria," anasema Bw. Mlilo.

### Mafanikio yaliyopatikana

Kuanzishwa kwa Kliniki za Sheria zilizoanza Mwaka 2024 nchini zimesaidia maelfu ya wananchi kupata haki zao kwa kutoa ushauri na msaada wa kisheria bila malipo, ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro 1,785.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akimuhudumia mwananchi wakati wa Uzinduzi wa Kliniki ya Sheria Bila Malipo Mkoani Singida.

Alisema misaada ya kisheria ambayo imetolewa na Kliniki imefanikisha kutatua migogoro ya ardhi, mirathi, na ndoa, ikipunguza mrundikano wa kesi mahakamani. Katika kuwahudumia wananchi waliopo maeneo mbalimbali, Kliniki imefikia wananchi 3,734,157, wakiwemo kwa kutoa elimu ya sheria na utawala bora.

Alisema tangu kuanzishwa rasmi Machi 2024, Kliniki za Sheria zimefanyika katika mikoa nane (8) ikiwemo Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Singida, Manyara na Simiyu. Alisema tofauti na Mahakamani Kliniki za Sheria zimekuwa zikitatua migogoro kwa njia ya maelewano, hivyo kuokoa gharama kwa pande zote zinazohusika.

Aidha, Kliniki hizi zimechangia kupunguza uhasama katika jamii na badala yake kujenga utengamano na mshikamano. Katika eneo la familia, Kliniki hizi zimefanikiwa kurejesha ndoa zilizokuwa zimevunjika ambapo ndoa zaidi ya 10 zimerudishwa na wanandoa kurejea kuishi pamoja kwa amani.

Vile vile, migogoro ya malezi ya watoto na matunzo imekuwa ikipatiwa suluhisho kwa njia ya maridhiano badala ya kulazimisha hatua za kisheria.

### Migogoro ya Ardhi na Mirathi yaongoza

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kliniki za Sheria zimebaini kuwa migogoro mingi inayowakumba wananchi inatokana na masuala ya ardhi na mirathi. Bw. Mlilo alisema sababu kuu zinazochangia migogoro ya ardhi ni pamoja na ukosefu wa uelewa, ununuzi wa ardhi bila kufanya uchunguzi wa kina, na vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya maafisa ardhi wasio waaminifu.

Alisema Kliniki za Sheria zilibaini maeneo mengi yasiyopimwa ni chanzo kikubwa cha migogoro kutokana na ukweli kuwa ardhi ni rasilimali yenye thamani kubwa na inayohitajika na watu wengi, hivyo ushindani wake umeongezeka kadri idadi ya watu inavyoongezeka.

Akizungumzia mirathi, alisema changamoto kubwa inatokana na wananchi kutoandika wosia. Alisema hali hiyo husababisha migogoro mikubwa baada ya kifo cha mmiliki wa mali, ambapo warithi huanza kugombania mali bila mwongozo rasmi.

Alisema pindi mwenye mali anapofariki, mali hizo huuzwa au kugawanywa bila mpangilio, jambo linaloathiri hata vizazi vijavyo. Bw. Mlilo alisema kuwa uandishi wa wosia na usajili wa mali ni hatua muhimu katika kuepuka migogoro.

Aidha alishauri wananchi kutumia mfumo wa "trust" ambao mwenye mali huandika na kupeleka Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) na pindi akifariki mali zake husimamiwa na Serikali. Alisema kwa kutumia mfumo huo warithi hawana mamlaka ya kuuza na kwamba njia hiyo ni bora kwa kuwa inalinda mali za familia na kuhakikisha zinanufaisha vizazi vingi.



Wakili wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bwana Silinde Gumada akitoa huduma ya ushauri wa Kisheria kwa mwananchi katika mojawapo ya Kliniki za Kisheria zinazoratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

> **"Anakuja mtu ana kesi yake unaisikiliza nyingi ni zile za Mabaraza ya Ardhi na za Mahakama ya Mwanzo unaona kabisa huyu alistahili haki lakini hiyo haki amepokonywa, wengine wana Mawakili wao na Wakili hakukata rufaa na bahati mbaya anakuja kwetu tayari muda wa kukata rufaa ulishaisha," alisema Bw. Mlilo.**

### Elimu ya Sheria kwa Umma

Mbali na kutatua migogoro, Kliniki za Sheria zimekuwa chombo muhimu cha utoaji wa elimu ya kisheria kwa wananchi. Alisema watu wengi wamekuwa wakihudhuria Kliniki hizo hata bila kuwa na migogoro, ambapo alisema wamekuwa wakifika kupata ufafanuzi juu ya masuala mbalimbali ya kisheria.

Elimu hii imewasaidia wananchi kuelewa haki zao, wajibu wao, na taratibu za kufuata katika kushughulikia masuala ya kisheria. Alisema hatua hiyo ni muhimu katika kujenga jamii inayoheshimu sheria na utawala wa sheria.

### Changamoto zilizopo

Licha ya mafanikio hayo, utekelezaji wa Kliniki za Sheria umekutana na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya watu wanaolalamikiwa kukataa kushiriki katika mchakato wa maridhiano na badala yake kubaki na msimamo wa kwenda Mahakamani.

Alisema hali hiyo hupunguza ufanisi wa Kliniki ambazo lengo kubwa ni kutatua migogoro nje ya Mahakama. Changamoto nyingine ni kesi ambazo tayari zipo Mahakamani ambapo Kliniki haziwezi kuingilia kati licha ya wahusika kuzileta ili zifanyiwe kazi.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu walipokea malalamiko ya baadhi ya Mawakili wasio waaminifu na watoa maamuzi katika Mahakama za Mwanzo na Mabaraza ya Ardhi ambayo husababisha watu kukosa haki hata pale inapoonekana wazi haki ni ya upande wake.

"Anakuja mtu ana kesi yake unaisikiliza nyingi ni zile za Mabaraza ya Ardhi na za Mahakama ya Mwanzo unaona kabisa huyu alistahili haki lakini hiyo haki amepokonywa, wengine wana Mawakili wao na Wakili hakukata rufaa na bahati mbaya anakuja kwetu tayari muda wa kukata rufaa ulishaisha," alisema Bw. Mlilo.

Alisema wakati mwingine kumekuwa na baadhi ya Mawakili wasio waaminifu ambao hawasimamii ipasavyo kesi ya mteja na matokeo yake ni kesi kushindwa.

### Mipango ya baadaye

Kwa mujibu wa Bw. Mlilo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imelenga kupanua huduma za Kliniki za Sheria katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma za msaada wa sheria.

Vilevile, wamelenga kuanzisha huduma ya simu bure itakayowawezesha wananchi kupata ushauri wa kisheria papo kwa papo bila gharama yoyote.

"Huduma ya simu ipo lakini kwa sasa unawasiliana na mtu mmoja ila itakayoanzishwa itakuwa na uwezo wa kuhudumia watu wengi kwa wakati mmoja, hivyo kuongeza ufanisi na kufikia wananchi wengi zaidi hata wale walioko maeneo ya mbali.

Bw. Mlilo alisema Kliniki za Sheria ni nyenzo muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa haki nchini kwa kutoa huduma za bure, kusikiliza wananchi, na kutatua migogoro kwa njia ya amani.

Mpango huo unatarajiwa kuleta matumaini mapya kwa wananchi wengi waliokuwa wakikosa haki kutokana na vikwazo mbalimbali na utapunguza migogoro, kuimarisha utawala wa sheria, na kujenga jamii yenye haki na usawa.